MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA

# Miaka minne ya Rais Samia na ukuaji wa soko la bima nchini

Na Na Mwandishi Wetu

KILA tarehe 19 ya mwezi Machi, ni kumbukumbu muhimu kwa nchi yetu, kwa kuwa taifa lilipata kiongozi mkuu, ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Machi 19, 2025 tunaadhimisha miaka minne ya uongozi wake ikiwa na mafanikio lukuki kwa ustawi wa taifa letu na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini ikiwa sehemu ya mafanikio hayo.

TIRA ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria ya Bima Sura 394.

Imepewa mamlaka ya kuratibu masuala yote ya kisera kuhusu bima ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, majukumu mengine ni kusajili na kutoa leseni kwa watoa huduma za bima, kuandaa na kutoa miongozo kwa watoa huduma za bima, kusimamia soko la bima nchini, kulinda haki za wateja wa bima na kuishauri serikali kuhusu masuala ya bima.

TIRA inajivunia uongozi makini wa Awamu ya Sita ambao umeendelea kutoa mchango kwa ukuaji wa sekta hiyo adhimu hapa nchini ukiwemo ushirikiano mahiri kutoka kwa viongozi wa juu ambao wamekuwa wakishiriki katika mikutano na midahalo mbalimbali ya Mamlaka na kutoa hotuba zenye kujenga kwa umma wa Tanzania.

Ndani ya miaka minne ya uongozi wake, TIRA imeendelea kujipambanua kama kiongozi wa mageuzi katika sekta ya bima nchini kwa kufanikisha yafuatayo :-

### Utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, inatoa haki ya msingi ya kila Mtanzania kuwa na bima ya afya bila kujali kama wanatoka katika sekta rasmi au isiyo rasmi.

Katika kutekeleza hilo, TIRA imepewa jukumu la kisheria kusimamia skimu zote za bima ya afya ili kuhakikisha watoa huduma wanafuata taratibu sahihi za usajili wa wanachama na pia kufuatilia utekelezaji wa huduma zinazotolewa ili huduma zinazotolewa ziendelee kuwa bora na za haki kwa wanachama walio kwenye skimu husika.

Mwaka 2024, kanuni kwa ajili ya kuanza kwa utekelezaji wa sheria hiyo zimetoka ambapo zinasisitiza juu ya usajili wa wanachama kwa uwazi na kuhakikisha michango inawasilishwa kwa wakati.

Katika kuchangia juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wa kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma bora za afya, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kwa kushirikiana na wadau, imetoa kadi za bima ya afya 3,000 kwa Watanzania wenye uhitaji ikiwa ni utekelezaji wa kauli ya Kamishna wa Bima Tanzania aliyoitoa ya kuchangia kadi za bima kwa Watanzania 10,000 ili waweze kupatiwa matibabu.

### Kuanzishwa kwa konsotia ya Bima ya Kilimo (Tanzania Agriculture Insurance Consortium)

Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu na takribani asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo kama chanzo cha mapato.




Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dkt. Baghayo Saqware

Hata hivyo, wakulima wanakutana na changamoto kubwa za kiuchumi na mazingira, ikiwa ni pamoja na mvua za kupindukia, ukame na maafa mengine.

Takwimu zinaonesha kwamba wakulima wengi nchini wanakumbana na hasara kutokana na majanga ya asili kama ukame, mafuriko, magonjwa ya mazao na wadudu waharibifu, jambo ambalo linahitaji mfumo wa bima ya kilimo.

Bima ya kilimo inatoa fursa kwa wakulima kupunguza athari za majanga hayo na inasaidia kukuza uzalishaji wa mazao na kuimarisha uchumi wa taifa.

Konsotia ya bima ya kilimo, huwapa wakulima unafuu katika kukata bima kwa makundi, lakini kila mmoja kunufaika pale linapotokea janga.

### Ongezeko la idadi ya Ofisi za Kanda za TIRA

Katika kuhakikisha wananchi wengi wanapata elimu ya bima, Mamlaka imeongeza wigo kwa kufungua ofisi za kanda ya Unguja na Pemba na hivyo kufanya idadi kufikia kanda 10 kwa upande wa Bara na Visiwani.

Zanzibar imeendelea kufanya vizuri katika sekta ya bima mathalani, katika Uzinduzi wa Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima kwa mwaka 2023 takwimu zilitolewa ambapo idadi ya watoa huduma wa bima kwa Zanzibar iliongezeka kwa asilimia 15 mwaka 2023 na kufikia watoa huduma za bima 92 ukilinganisha na watoa huduma wa bima 80 waliosajiliwa kwa mwaka 2022.

>> INAENDELEA UK. 5

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA

# Miaka minne ya Rais Samia na Ukuaji wa Soko la Bima



Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 15.0. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa kwa upande wa kampuni za bima hadi kufikia mwaka 2023, kulikuwa na kampuni 17 za bima zilizofungua matawi Zanzibar, zikiwemo ICEA Lion, Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), Shirika la Bima la Taifa (NIC), Bumaco, Strategis, UAP, Sanlam Life, Heritage, Milembe, First Assurance, Mo Assurance, Tanzindia, ZIC Takaful, GA, Reliance, Mayfair, na Jubilee Allianz. Kampuni hizi zinatoa huduma za Bima za kawaida, Bima za Maisha, Bima za Afya na bima nyingine.

**Mageuzi ya Kisera na Kisheria**

Ndani ya kipindi cha miaka minne ya Rais Dk. Samia, TIRA imezindua miongozo na sera zinazolenga kuboresha mazingira ya kisheria kwa watoa huduma za bima na wateja.

Hii ni pamoja na kuongeza uwajibikaji wa kampuni za bima kuhakikisha fidia zinalipwa kwa wakati.

Kwa kushirikiana na taasisi za serikali, TIRA imehakikisha kwamba mali za umma zinalindwa ipasavyo kupitia bima, hatua inayochochea uwajibikaji wa kifedha na kupunguza mzigo wa gharama kwa serikali.

Mfano wa miongozo iliyotolewa kwa mwaka 2024, ni pamoja Miongozo ya Bidhaa za Bima, Miongozo ya Wakaguzi wa Nje wanaohudumia sekta ya bima na muongozo wa ukokotoaji na ukusanyaji wa tozo za ada za bima.

**Ubunifu katika Sekta ya Bima**

Ubunifu umekuwa sehemu muhimu katika kuendeleza soko mathalani mwaka 2024 pia umeona kuzinduliwa kwa huduma mpya za bima zinazolenga mahitaji ya kipekee ya wateja.

Mojawapo ya mafanikio makubwa ni kuzinduliwa kwa huduma za Takaful, ambazo zinafuata misingi ya Shariah.

Uzinduzi huu umeimarisha zaidi utoaji wa huduma zinazojumuisha makundi tofauti ya dini na tamaduni.

**Uzinduzi wa Taarifa ya utendaji wa soko la bima ya kila mwaka**

Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima hufanyika kila mwaka na kwa kipindi chote cha uwepo wa Rais Dk. Samia madarakani tukio hilo lilifanyika kwa kutoa mchanganuo mbalimbali katika soko mfano idadi ya watoa huduma au huduma zilizoongezwa.

**Taarifa hizo pia zinapatikana katika tovuti ya TIRA.**

Uzinduzi wa Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima kwa mara ya mwisho ulifanyika Novemba, 2024 kwa kutoa taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima kwa mwaka 2023 na kuhudhuriwa na watu zaidi ya 400 huku watu zaidi ya 1,000 wakifuatilia mbashara kupitia mtandao wa YouTube wa Mamlaka.

**Taarifa hii imeonesha kukua kwa soko kwa kiwango kikubwa kama ifuatavyo;-**

Ada za Bima (Gross Premiums Written - GPW) zimepanda kwa asilimia 7.4 hadi kufikia Sh. trilioni 1.24, kutoka Sh. trilioni 1.17, watoa huduma za bima wameongezeka kwa asilimia 33, na kufikia 1,549 ikilinganishwa na 1,164 mwaka uliopita.

Aidha, madai ya bima yaliyolipwa yameongezeka kwa asilimia 25.5, hadi kufikia Sh. bilioni 488.2 kutoka Sh. bilioni 389.

Kiwango cha mali za bima kimeongezeka kutoka Sh. trilioni 1.7 hadi kufikia Sh. trilioni 2.15 huku uwekezaji pia ukiongezeka hadi Sh. trilioni .1.27 kutoka Sh. trilioni 1.17.

Fursa za ajira zimeongezeka kwa asilimia 34.1, ambapo jumla ya ajira 5,595 zimekodiwa mwaka 2023. Aidha, kiwango cha ubakizaji wa bima za kawaida (general insurance retention) kimeongezeka kutoka asilimia 49.4 hadi asilimia 55.5 huku kiwango cha ubakizaji wa bima za maisha kikiwa ni asilimia 83.2.

**Maonesho ya Kimataifa na Ushiriki wa TIRA**

TIRA imeshiriki katika maonesho makubwa mbalimbali yakiwemo ya Nane nane, maonesho ya ushirika, maonesho ya madini, manesho ya Biashara Zanzibar, maonesho ya Tanzanite Manyara na maonesho ya wiki ya fedha, mathalani katika maonesho ya saba saba jijini Dar es Salaam 2024, TIRA na wadau wa sekta ya bima, ilizindua "Kijiji cha Bima" ambapo wananchi walipata fursa ya kujifunza kuhusu huduma za bima kupitia njia rahisi na shirikishi.

Kijiji hiki kimekuwa mfano wa ubunifu wa kuifikisha bima kwa kila mmoja, huku kikionesha dhamira ya TIRA ya kuimarisha elimu ya bima kwa Watanzania wote.

**Maono ya TIRA kwa Soko Salama la Bima**

Kwa mwaka 2024, TIRA imeendelea kuimarisha mifumo ya kidijitali inayowezesha usajili wa bima, ulipaji wa fidia kwa wakati na usimamizi wa masuala ya kisheria kwa uwazi zaidi.

Mfumo huu unalenga kujenga imani miongoni mwa wateja na watoa huduma huku ukihamasisha ukuaji wa sekta ya bima nchini.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi imara ndani ya miaka minne, TIRA inaendelea kusimamia maono endelevu kutoka kwa serikali na wizara ili kuleta mageuzi mbalimbali katika soko la bima nchini.

